JUA

GAZETI LA MAENDELEO

Kiongozi: Mutiri-wa-Bashara - Mwaka wa 21 - Toleo la 449

Kifo cha Ndadaye, mapinduzi kwa damu

Jaribio la kuipindua serkali iliofanyika na kundi la askari-jeshi nchini Burundi yalainiwa na mataifa ulimwenguni pia laonekana tu la ukabila. Na kosa la kumpindua na kumuuwa Ndadaye halijulikane. Habari zajulisha kuwa bwana Ndadaye kanaswa ndani ya nyumba yake siku ya tatu, tarehe 20/10/1993 usiku na kuuwawa kesho yake.

Wanaotajika kuhusu kitendo kile haramu ni mabwana Jean Baptiste Bagaza na Cyprien Mbonimpa waliokuwa hapo zamani rais wa Burundi na waziri wa mambo ya inje wa serkali ya Buyoya, ila habari zingine zakanusha mashtaki yale. Lakini waliohusika halisi ni mabwana Bizuru (major), "lieutenant-*colonel*" Jérome Sinduhije aliyekuwa balozi wa Burundi mjini Kinshasa. Wote hao wasemekana kuwa wazaliwa wa Burundi (Bururi) ambao ni *Watutsi*.

Maaskari na raia waliotajika ni Pascal Simbanduku, *Rumbete*, Busokoza, Hilaire Ntakingiza, Kamana, Haziyo, Antoine Nimbeshe, Gerard Shishahayo, Ndihisaba, Ndacosaba, Nkurunziza, Niyonkuru, Alphonse Kadege (aliyekuwa waziri wa Buyoya), na Charles Mukasi ambaye ni mwanahabari huru.

Labda bwana Ndadaye kauawa kwa vile, kwanza, katoa amri ya kuwasamehe wote waliokuwa wakifungwa kufuatana na matendo maovu, tena kapendelea kutumika na kila moja. Kosa lingine, bwana Ndadaye kaondoa kwa haraka.

Mabalozi na wafanyakazi wakuu wa serkali huko akisahau namna jeshi lilivyoundwa. Kufuatana na kitendo kile cha uuaji kilichochukiwa na mataifa yote ulimwenguni, nchi ya Burundi yakabiliwa na shida ya vita ya wenyewe kwa wenyewe. Ndio sababu vikosi vya askari-jeshi vya kimataifa (forces internationales) vyajaribu kuleta amani nchini Burundi. Ingawaje hali ya mambo yasemekana kuwa sasa ya matumaini, habari toka Bujumbura zaeleza kama kabila hizo mbili, Wahutu na Watutsi zauwana na hata ngombe za Watutsi zakabiliwa na shida ya kupata nafasi ya malisho.

Tatizo la ajabu ni kuona watu yapata karibuni milioni 1 wamekwisha kukimbia Burundi na kuenda uhamishoni nchini jirani za Tanzania, Rwanda, Zaïre 50.000) na mahali mengineo. Huko walipo wakiwa na tatizo la kupata chakula, dawa na mahali pa kukaa.

Nchini Bujumbura Wahutu wajitolea kufa wote ikiwa wauaji wale hawatahukumiwa vikali. Ingawaje katibu mkuu makamu wa umoja wa mataifa na yule wa umoja wa nchi huru za Afrika katembelea Burundi kusudi ya kujionea mwenyewe hali ya mambo, wakaaji waomba serkali ya waziri mkuu bibi Sylvie Kinigi kuzibiti usalama na kuendesha mambo inivyostahili. Kwa wakati mwengine serkali hiyo yahusika na mazishi ya raïs Ndadaye na wengineo namna inavyostahili na heshima zote, huko Ndadaye abaki katika historia ya Burundi kuwa "héros national".

Yanayobaki ni kujiuliza namna gani kabila hizo mbili zitaendelea kuishi pamoja wakati zajiona kuwa maadui kidamu ? Angalisho, moto huko utazimwa ?

Mutungwa Abandelwa Phély

Shirika la SNEL liaminiwe ?

Kutokana na matatizo linalo Shirika linalohusikalo na utoaji na uchuuzi wa moto wa stimu ama Snel na wa "clients" wake, ujumbe toka uongozi mkuu wa shirika hilo mjini Kinshasa na ukiongozwa na bibi Tokwaulu Aisa, ujumbe huo ulikutana katika masimulizi na wakaaji mijini Goma, Bukavu na Uvira. Wajumbe waliwasikia wakaaji na kujibu kwa maulizo waliyotoa. Hasa kuhusu malipo ya stakabazi (factures) zatumwa, ukosefu pia kukatwa kwa moto mara nyingi.

Kuhusu malipo, ilionekana kweli kuwa malipo yapaswa kuwa ya mitindo ifuatayo : Hayo ya mashirika makubwa, ya viwanda na hayo ya matumizi wa moto huo manyumbani. Ila kweli kutokana na ukosefu wa vifaa ao vyombo vya kuonya utumizi wa moto kama vile "compteurs" shirika la Snel lalipisha kiasi cha feza lawaza bila kujali ni nani atumiwa stakabazi. Ni hapo imehaidiwa kuwa kutachunguzwa upya malipo na vifaa vya uchunguzi wa utumizi wa moto vitaharikishwa baadae.

Kuhusu ukosefu wa moto ama kukatwa kwa moto huo, imejulishwa kwa vyombo vyatumimiwa kwa sasa, vingi vimekwisha kuzea na watumizi wa moto huo wa stimu wengi wao wameuchukuiwa kwa magendo. Hata waitwa wa "dahuleurs" kwa nginsi vyombo vyaungua ajabu na baadae mahali kulitukia msiba yakosa moto. Na shirika Snel kutokana na ukosefu wa feza za kutoshelea kwa kuuza vingine vyombo vipya lajiona mbele ya matatizo makubwa. Kwani yafaa kweli moto uongezeke. Kwa hiyo bwawna (barrage) la moto la Ruzizi I laendelea kutengenezwa upya, la Ruzizi II kuongezwa na wataalam hujifunza namna ya kusimika bwawa lingine Ruzizi II. Toka hiyo yafaa basi wa "clients" wa shirika Snel wasikie na wawe watulivu na hakika kuwa lahusika na mahitaji yao na lajitaidi kuwafurahisha siku zijazo. Kwa hiyo, yafaa kweli kila "client" alipe feza apaswa kwa shirika Snel. Ni kwa namna hiyo tu ataweza kushiriki kwa maendeleo ya shirika hilo na ya jimbo nzima.

André Bisimwa L-B Tserou

Neno la wasomaji

Itombwe yasonga mbele

JUA mpenzi,

Nikiwa mmoja kati ya wasomaji wako watukufu, nafurahiwa sana na Gazeti letu "JUA" kwa kuwa latujulisha mambo yapitayo katika jimbo letu, nchini Zaïre na duniani kwa jumla. Ni toka hiyo ningependa kukufahamisha machache juu ya hali iliyoko mkoani mwetu Itombwe sasa.

Ikiwa moja kati ya mikoa yaunda mtaa wa Mwenga, kiasi kikubwa cha eneo lake ni mwitu ambamo mwapatikana mali mengi. Ni kama vile madini (zahabu na mengineo) bali pia mazao ya mlimo. Lakini ubovu wa mabarabara haturuhusu kusafirisha mavuno ginsi ifaavyo mijini mikuu kama vile Uvira, Baraka, Bukavu,...

Kwa kweli baada tu ya kukabizwa madaraka ya uongozi wa mkoa wa Itombwe, bwana Kitabu Kininga, kiongozi huyo mpya ajitatanua kurudisha ukimya, amani na usalama na toka hayo kustarehesha maendeleo mkoani na upate kusonga mbele. Hiyo yatokana na masikilizano kati yake na askari-jeshi na kuungwa mkono na wakaaji. Ambao walijitahidi kufungua njia na kujenga upya barabara hadi Kalembelembe/Fizi ingawa shirika la mradi SIDEM katudanganya kama itatutengenezea barabara kupitia Mwenga. Pia wakaaji na kiongozi huyo waanza kujenga vyumba kazaa vya kazi. Misaada katolewa imepeperushwa na wanaohusika wamoja.

Kupitia kwako, mpenzi JUA, twatoa mwito kwa wazaliwa wote wa Itombwe, wachuuzi, viongozi wa makanisa, wanamiradi na hasa kwa serkali kutuunga mkono tupate kusikia utamu wa siasa yahitajika katika Jamhuri ya Tatu. Twaomba pia muwe munatutumia gazeti zakuuza kwani tupo wengi tunayo hamu ya kusoma "JUA".

Wako msomaji,
Wissoba Lusambya
mkaaji wa
Mikenge/Itombwe
mtaani Mwenga

NLW : Ndugu Wissoba, tumefurahiwa na kibarua chako na twatumaini ombi lako litapata jibu siku za usoni.

UHARIRI

Watutakia nini ?

Siku kwa siku uwasiwasi watezamiwa nchini Zaïre kutokana na hali ya siasa pia na ya uchumi iliyoko.

Kwa kweli, hatujui wanasiasa wajifikiri nini juu ya matatizo ya kisiasa, kiuchumi na ya kijamii yawateketeza raïa. Kwa kuwa hakuna hadi leo matumaini yatezamiwa kwa kupata majawabu kwa magumu yasonga wananchi. Wote tulikuwa tukingojea kwa hamu matukio ya Mkutano mkuu wa kitaifa na ambayo tulizania ndio yatatuonya njia bora kwakufikilia wokovu wa wote wakaaji. Lakini baadae, wanasiasa ambao wagombania viti, vyeo na madaraka kwa manufaa yao wenyewe kaleta vurugo na watakakuonya kwa wote wanahusika kuwa makosa yalikuwa bado katika hati za matukio hayo. Serkali zabadilishwa mara, viongozi watengwa madarakani na hawa wajionya hapo hapo wapinzani wakuu na wakali kwa wenzio wateuliwa. Ingawa Mwana-Zaïre ahitaji usalama, amani, uhaki na kazalika irudishwe. Basi kwa kifupi, urahisi wa maisha mazuri yastareheshwe. Masimulizi na mabishano kati ya wanasiasa hayafanikiwe. Zaidi ya hayo, wanasiasa wamoja wapinga mabadilisho ya feza kafanyika.

Kulingana na hali hiyo, mafasirio yatolewa kuhusu feza mpya, yasemekana eti hayaaminiwe na wapinzani hata na wakuu makanisani.
Hawa wasema kutolewa kwa feza hizo mpya ni kwa nia tu ya kuangamiza kwa lote raïa na nchi kulazwa kichalichali. Kwa ngambo yao, viongozi nchini kwa sasa, wakazania na kusisitiza kuwa feza mpya zina samani kubwa (dolari 330 kwa zaïres 100 kwa sasa ingawa leo hii dolari ni 100 ni miliari moja na nusu kwa feza za zamani). Kuambatana na sheria n˜003/93 katiwa sahihi na Raïs wa Jamhuri mnamo tarehe 28 septemba 1993 na kujulishwa mnamo tarehe 22 oktoba 1993, zaïre 1 mpya ina samani ya zaïre 3.000.000 ya zamani, zaïre 5 : zaïre 15.000.000, zaïre 10 : 30.000.000 ya zamani. Likuta 1 ni zaïre 30.000 ya zamani, makuta 5 : zaïre 150.000, makuta 10 : zaïre 300.000 na makuta 50 : zaïre 1.500.000 ya zamani.

Feza hizo mpya, wasema serkalini, ni za lazima sana na zitaweza kuwa jawabu kwa matatizo yaliyoko. Ni kama vile ukosefu wa feza kwenyi mabenki, malipo ya mishahara ya wafanya kazi, kuruhusu mabenki kutumika upya kazi zao nginsi ifaayo na kuimarisha mavuno. Hatua kali zimechukuliwa na serkali ili feza hizo zikubaliwe na zipate kutumika.

Ingawa hatua hizo kachukuliwa, wapinzani wa Raïs wa Jamhuri na wa serkali wajitatanua kuhimiza watu wasikubali feza hizo mpya kwani wahakikisha kuwa utumizi wa feza hizo ni raïa kujitia kamba.shingoni na maisha kuzorota. Hapa kwetu jimboni mwa Kivu ya kusini, mwanasiasa Ferdinand Chimanuka Ntagaya Ngabo, prezidenti wa chama PDSC na wa Umoja mtakatifu wa vyama vya upinzani mkali katiwa nguvuni kwa amri ya Korti kuu jimboni mnamo tarehe 23 oktoba 1993 na nakuelekezwa mjini Kinshasa mnamo tarehe 25 oktoba 1993 apate kusikilizwa na waamzi pia viongozi na wakuu serkalini. Huyu ashtakiwa kataka kuleta fujo na vurugo kwa masemi na maandishi nchini et i feza hizo mpya hazina maana na viongozi kwa sasa wana nia tu ya kuiba raïa. Miongoni mwake aungwa mkono na wanasiasa, wamini, wadini, viongozi wa mashirika ya kiraïa kazaa ambao kaomba kwa raïa wote kugoma kazi ili mwanasiasa huyo afunguliwe na aachwe huru. Si yeye tu bali pia gazeti "Umoja" na "La RÇfÇrence" kapigwa bakora na kukatazwa kupasha habari muda wa miezi kaa. Kwani angalisho kapewa na waziri mkuu Faustino Birindwa kwa yeyote atakayejiruhusu kushawishi wakaaji kukataa feza hizo mpya ataazibiwa vikali kulingana na sheria. Kesho zamu ya nani ?

Basi Raïa hujiuliza kuwa wanasiasa watutakia nini kw kuwa tukwisha kuteswa na kuangamizwa na magumu kazaa. Hawa wamashindwa kabisa kupata jawabu kwa matatizo ya kisiasa, ya kiuchumi nakijamii yatukumba. Kumbe wao ndio msinji wa hali ya ubovu tunayo kwa sasa. Ingawa wote wajidai kuwa wataalam katika mambo fulani fulani, walimu wakuu, madaktari na wenyi maarifa mengi. Hiyo ndiyo mshangao mkubwa watushika. Basi tungojee kwani kuambiwa kuna uongo tukajionee wenyewe yatakayo tukia.

André BISIMWA L-B Tserou

Je, umesikia ... ?

KUWA, kwa nia ya kuheshimisha amri ya kiongozi wa jimbo la Maniema ambaye ashurtisha viongozi wa mitaa na mkoa wa Kakutya kamutolea kiasi kingi cha pesa, bwana Kansilebo katoa amri ambayo ni ya kipekee mtaani mwake ? Eh, bwana huyo kanena kuwa ndoa yoyote isiyo na vikartasi vya utambulisho na kujulikana kiserkali (contrat de mariage) kwa chumba chake cha kazi, yapaswa kutoa "amende" ya "convocation" ya milioni 50 ya zaïres baada ya kulipa kwanza pesa za "convocation" ao za "mandat". Bila hivyo, "contrat" ile ya ndoa haitajulikana kiserkali.

KWAMBA, yapata karibuni miaka kumi hivi, sehemu moja ya askari-jeshi na wafanyakazi wa serkali walikuwa wakila nyama hata mara sita kwa juma kwa vile nyama ilikuwa ikiuzishwa kwa bei rahisi kwao kuliko wengine hapa mjini Bukavu ? Hao, ni wale waheshimiwa wa jamhuri zote mbili. Yasemekana kuwa, tangu tarehe 29/10/1993 hatua hiyo kapigwa marufuku kunako soko kuu la Kadutu kupitia mwenyekiti wa mji wa Bukavu, ndugu Migale Mwene Malibu, ambaye kasikia malalamiko ya wachinja nyama. Bei ya nyama imepangwa namna moja kwa wa askari na wafanyakazi wengine wa serkali ambao wanunua sasa kwa bei ile moja iliyoko sokoni. Hata hivyo, twajiuliza kwa nini wakuu wa askari-jeshi, wa mji wa Bukavu, wa kuchunguza bei, na wale wafanyabiashara kangojelea muda wa miaka 10 yote ile ! Wangwana husema : "kinywa kilichonyonya hakiwezi kusahau utamu wa maziwa". Ni kweli kuwa waheshimiwa hao watatii hatua ile ? Hum !